*Kioo cha Lugha* 2, 1996/97:71-80

# Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia Katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi

*Clara Momanyi**

## 1. Nadharia ya uchanganuzi - nafsia katika mtazamo wa kike

Chanzo cha uhakiki wa masuala yahusuyo mtazamo wa kike (*feminism*) ni harakati za ukombozi wa mwanamke. Masuala ya mtazamo wa kike yanahusu mapambano ya kuondoa unyanyaswaji wa mwanamke katika misingi ya kijinsia. Katika uhalisi wake, mtazamo huu unahusu harakati za kufutilia mbali itikadi za kijamii zilizoimarishwa chini ya misingi ya uana, na ambazo humweka mwanamke katika nafasi duni akilinganishwa na mwanamume. Ni harakati za kuunda upya mitazamo ya jamii dhidi ya nafasi ya mwanamke.

Nadharia kadha za uhakiki wa kifasihi zimependekezwa katika uchanganuzi wa matini za kifasihi. Si jukumu la makala kuzipitia nadharia zinazoshughulikia masuala ya kike. Jukumu kuu hapa ni kuteua mojawapo ya nadharia hizi na kuona jinsi inavyoweza kutumiwa kuchanganua kazi za kifasihi.

Katika makala jinsia imechukuliwa kumaanisha kitengo cha maumbile ilhali dhana ya uana imechukuliwa kumaanisha kitengo cha kijamii. Kwa hivyo, dhana ya uana imeibushwa na jamii ili kuimarisha tofauti ya majukumu kati ya mwanamume na mwanamke.

Takriban kila kazi ya kifasihi ina kipengele cha uana. Aidha katika jamii mbalimbali, mtu anapoitwa mwanamume au mwanamke huwa amewekwa katika kitengo fulani cha kijamii. Katika kila kitengo, kuna itikadi na falsafa zinazomiliki mahusiano katika kitengo chenyewe, na kadhalika maingiliano yake na kile kingine.

Nadharia ya uchanganuzi - nafsia katika mtazamo wa kike (Feminist Psychoanalytic Theory) ina chanzo chake katika kazi zilizoasisiwa na Jacques Lacan. Nadharia hii inayohakiki matini katika misingi ya uchanganuzi - nafsia, huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa

* Mhadhiri, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta

kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume.

Katika huu utaratibu fiche, maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke kwa mfano, hugubikwa na badala yake, maumbo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusiano wowote na uhalisi wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususan kupitia kwa lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu nafsi ya mwanamke imefungamana na lugha anayozungumza, lugha inayoashiria uana wake. Nafsi hii hufinyangwa na jamii kupitia asasi mbalimbali ili iweze kukubalika katika utaratibu huo wa kiishara. Uchanganuzi - nafsia katika mtazamo wa kike basi, ni nadharia bia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya uana.

Katika mtazamo huo wa kinafsia, neno "mwanamke" ni ishara bali siyo nafsi yake halisi. Maana ya neno hili huyakinishwa na mila au utaratibu wa utamaduni husika. Mclaughlin (1990: 155) kwa mfano, hakukosea aliposema kwamba dhana ya mwanamke kwa uhalisi wake ni dhana ya kisiasa. Haielezi uana pekee bali inaeleza pia hadhi au nafasi yake katika jamii.

Kulingana na mtazamo wa Lacan pia, maana na utaratibu wa kiishara hujengwa chini ya taasubi ya kiume inayohimili tofauti zote za kiuana katika mfumo wa kuumeni. Taasubi ya kiume ndiyo inayoashiria nguvu (power) na huhusishwa na nafsi ya kiume. Shauku katika uongozi na umilikaji wa mwanamke ndivyo vinavyobainika katika ile nafsi ya kiume ambayo huwakilishwa kiishara na taasubi ya kiume.

Katika mwelekeo huu basi, mtoto wa kike anapokua, hufanywa kuamini kwamba yeye ni kiumbe duni mbele ya mwanamume. Hili hudhibitiwa moyoni mwake daima. Hapa ndipo anapochukua nafsi bandia, tofauti na ile yake halisi. Hili huathiri tabia na hulka yake. Itikadi za kuumeni humuunda mwanamke katika hali ambazo zinaweza kutimiza matakwa ya mfumo huo wa kuumeni. Nguvu za kike (female libido) hudidimizwa na utaratibu wa kuumeni ambao pia humsawiri mwanamke kwa namna zinazomfanya apoteze ile asili yake halisi.

Katika muktadha wa uhakiki wa matini za kifasihi basi, nadharia hii inaweza kutumiwa kwa kuzingatia kwamba lugha haiwakilishi uhalisi bali ni

utaratibu wa kiishara. Kwa hivyo, taswira za wanawake katika fasihi aghalabu haziwakilishi uhalisi wao bali ni taswira bandia zilizosheheni ishara za uana, hususan katika matumizi ya lugha. Aidha, uhakiki huo una wajibu wa kuzingatia kuwepo kwa taasubi za kiume zilizoimarishwa ndani ya utaratibu wa kiishara katika mfumo wa kuumeni (patriarchal symbolic order). Taasubi hizi ndizo zinazomdunisha mwanamke na kumweka katika kitengo maalum kijamii.

Katika mkabala huu, makala hii inahakiki tamthilia ya Mwachofi (1987) iitwayo *Mama Ee* ili kuona jinsi masuala yanayojadiliwa yanavyoweza kuchanganuliwa kulingana na nadharia hii.

## 2. Uhakiki

### 2.1 *Tamthilia kwa Ufupi*

Huu ni mchezo unaozungumzia harakati za ukombozi wa mwanamke kutokana na ugandamizaji wa mwanamume. Aidha, unasawiri mapambano ya mwanamke dhidi ya mila na itikadi za kale na za kisasa zinazomdhalilisha mwanamke, na kumnyima nafasi ya kuutambua utu na uhuru wake.

Kupitia kwa mhusika mkuu Mwavita na dadake Tenge, mwandishi anatuchorea picha halisi ya dhiki za aina mbalimbali zinazowakumba wanawake katika jamii ya leo. Bila shaka jumuiya inayozungumziwa ni jumuiya iliyokumbatia mfumo wa kibepari uliosheheni itikadi za kuumeni. Hii ni kutokana na matukio ya mchezo wenyewe.

### 2.2 *Asasi ya Ndoa*

Ndoa kati ya Kinaya na Mwavita ni kielelezo cha ndoa kama inavyoeleweka ndani ya mfumo wa kuumeni. Mwandishi anatoa taswira mbili za ndoa ya Wahusika hawa; ndoa yao chini ya sheria za kienyeji na ndoa hiyo chini ya kanuni za kanisa. Picha zote mbili zinabainisha uduni wa mwanamke katika asasi hiyo.

Taasubi za kiume zinazoendelezwa kupitia mhusika Kinaya ndizo zinazomdhalilisha Mwavita. Kinaya ni kelelezo cha wanaume waliolelewa ndani ya mfumo wa kuumeni ambao licha ya kwamba wameelimika, bado wanashikilia kwa dhati dhana ya "mwanamke" kuwa ni kiumbe cha kumtumikia mwanamume, kumnyenyekea na kumtii (uk.3). Mwavita anatarajiwa kumsubiri mumewe mlangoni na kumpokea bila kujali wakati anapowasili (uk.31).

Katika muktadha wa utumishi huu, Kinaya hasiti kumkumbusha mkewe kuwa alimlipia mahari, kwa hivyo ni wajibu wake kumtumikia:

> Mimi ni mume wako na ndiye mwenye amri katika nyumba hii yangu. Lazima ufanye nisemalo. Usifikiri hiyo elimu yako na kazi ya mshahara imekufanya mume sawa na mimi ..... (uk.3).

Dondoo hii linaonyesha kwamba elimu ya mke haina nafasi mbele ya utaratibu huu wa kuumeni. Uduni wa mke lazima uzingatiwe hata kama amefikia kilele kipi cha elimu.

Umilikaji wa mwanamke pia unadhihirika wazi (uk.4) kinaya anapotamka kwamba mwanamke hana chake. Kipengele cha mahari kinashadidia umilikaji huu. Katika uasili wake, mahari ilitumika kama ishara ya kuunganisha familia mbili ambazo zinaimarisha undugu kutokana na ndoa. Kadhalika, ni zawadi wanayopewa wazazi wa msichana baada ya kutekeleza kazi nzuri ya kumlea binti yao. Hapa dhana ya ununuzi haikuwa kusudio. Mahari yalitolewa kufidia pia pengo aliloacha msichana hususan katika huduma alizotoa.

Kwa upande mwingine, mahari ilikuwa njia moja ya kumfunga mwanamke kwa mumewe. Ni sawa na kumvalisha pingu za utumwa na kumwekea uzio wa utumishi. Hii ni kwa sababu baada ya kuolewa, mwanamke hakuwa na mamlaka au nguvu za kutoa maamuzi hasa katika familia za Kuumeni. Mwanamke alichukuliwa kama sehemu ya mali ya mumewe. Hivi ndivyo mhusika Kinaya (uk.4) anavyoona pia.

> Katika zama hizi zetu, wanawake wanachuuzwa kama bidhaa sokoni. Kinaya anakiri haya (uk.4) anapomwambia mkewe kwamba "Baba zetu siku hizi wanawauza. Mimi nililipa shilingi elfu mbili zaidi kwa kuwa ulifika kidato cha sita.....".

Mwanamke hana mamlaka hata juu ya umilikaji wa wanawe (uk.6).

Dhana ya mwanamke kama chombo pia inabainika kupitia usawiri wa matendo ya wahusika Kinaya na George. Wahusika hawa ni vielelezo halisi vya wale wanaume wanaomchukua mwanamke kama chombo cha kutimizia ashiki za kiume. Tenge anakuwa muhimu kwa George pale tu anpomtimizia haja zake. Kulingana na Kinaya pia, wanawake wote ni maua tu. Hii ndiyo maana anawabadilisha kama nguo. Taswira ya pambo (uk. 49) inabainika pia pale Kinaya anapomtaka mkewe waandamane naye shereheni. Mke

anapoghairi, anamwambia kuwa atapata maua mengine huko shereheni. Dhana ya mwanamke kama kiashiria cha pambo imesakini katika mfumo wa kuumeni. "Mwanamke" huashiria pambo la kuajabiwa na kufurahisha, mfano wa sanamu ya kuchongwa.

Lugha inayotumiwa na Kinaya pia inaashiria nguvu na mamlaka ya kiume, tofauti na ile inayotumiwa na mkewe. Kwa mfano, Kinaya anamwita mkewe hawara na kumtolea matusi (uk.7). Mkewe hahiari kumrudishia mumewe matusi bali anamjibu "Aah! Kinaya ndugu yangu! Wanidharau hivyo". Mfumo unaojadiliwa haustahimili lugha ya matusi kutoka kwa wanawake. Hata hivyo, kutokana na uhasidi wa mumewe, mwavita hasiti kuyatumia matusi ili kupigania utu wake (uk. 90).

## 2.3 *Asasi ya Dini*

Dini kama vile Ukristo na Uislamu zimetumiwa kuhalalisha mfumo wa kuumeni. Dini hizi zilizoanzishwa ndani ya mfumo huu zina taathira kubwa katika maisha ya mwanamke. Taathira hizi zinadhihirika katika tamthilia ya Mama Ee.

Tumeonyeshwa jinsi kimbelembele cha mwanamke kilivyomchongea (uk.18). Katika muktadha wa tamthilia hii pia, taasubi za kiume zinazoendelezwa na mhusika Padre (rafikiye Kinaya) zinamdhalilisha Mwavita (uk. 62). Kulingana na Padre, ndoa ni Sakramenti kubwa ya kanisa la Mungu hapa duniani. Anaendelea kusema Mwavita na Kinaya waliunganishwa kuwa mwili mmoja, roho moja siku walipofanya ndoa. Kwa hivyo Mwavita anapojitenga na Kinaya, anavunja sheria ya Mungu. Kule kuvunja ndoa ya Mungu ni kitendo cha uovu (uk. 63). Hapa tunaona mafundisho ya Biblia yakitafsiriwa vibaya kwa manufaa ya mwanamume.

Kwa mfano, Biblia haisemi kuwa watu wakioana wanakuwa roho moja. Kila binadamu ana roho yake binafsi inayowajibika kwa Muumba wake. Tahadhari anazotoa Padre basi, zinadhamiria kumtia Mwavita woga, aghairi na kumrudia mdhulumu wake - Kinaya. Vitisho vya kidini dhri ya mwanamke tunavikuta pia katika Uislamu ambapo mwanamke anashauriwa amtii mumewe ili apate kibali cha kuingia peponi (Taz. Utendi wa Mwanakupona, ubeti 27).

Kadhalika, tunamwona Mwavita akiuasi mfumo ulioko na kuutaka uhuru wake (uk. 59). Kutokana na hili, kanisa linamtenga na kumkataza kupokea Sakramenti (kipaimara). Kwa upande wake, Tenge anatengwa na kanisa kwa

kuwa amepata mtoto nje ya ndoa. Anaambiwa kwamba mwanawe hatabatizwa (uk. 63) kwa sababu ni mwana haramu.

Bila kujali yale yaliyofanywa na George, mpenzi wa Tenge, jamii inamwadhibu. Tenge na Mwavita wanakuwa majeruhi wa jamii. Mwavita anayeasi utaratibu wa jamii unaomtaka aucheze mchezo aliofunzwa jukwaani tangu akiwa mdogo, anaitwa muasi. Wanawake mitaani wanaambiwa wasiandamane na Mwavita, la sivyo hawatapata waume.

Wanawake wanaodhihaki na kumsuta Mwavita ni wale waumini wa mila za kijamii zinazowataka wamtunze, kumtumikia na kumvumilia mwanamume bila lalamiko lolote. Haya pia ndiyo yanayomkuta Lanina wa Kilio cha Haki kwani anaitwa malaya kwa sababu anajiunga na wanaume kwenye mapambano ya kisiasa na kutupilia mbali majukumu yake kama mke nyumbani. Huku ni kuvunja miiko ya jamii na matokeo ni kumfanya mwanamke aitwe muasi.

### 2.4 *Asasi ya Sheria*

Kupitia kwa matukio ya Mama Ee, ni dhahiri kwamba asasi ya sheria iliyoimarishwa ili kuwatumikia wanajamii, ina ubaguzi wa kiuana. Asasi hii inayosimamiwa na kuongozwa na wanaume, haijali shida zinazowapata wanawake hususan katika ndoa.

Kwa mfano, mahakama inatumiwa kubainisha nguvu na mamlaka ya mwanamume. Uamuzi wa mahakama haufui dafu mbele ya utaratibu wa mfumo wa kuumeni. Hii ni kwa sababu ingawa Kinaya anakatazwa na mahakama asiende kumsumbua Mwavita kwake baada ya talaka, tunamwona Kinaya akiendelea kumsumbua Mwavita. Hata kabla ya talaka kutolewa, Polisi wanamsuta Mwavita (uk. 67) na mwishowe kumwambia hawawezi kuingilia mambo ya "family". Tunamwona Mwavita akikimbilia usalama wake kwenye kituo cha Polisi ili kujinusuru na mapigo ya mumewe lakini hapati usaidizi wowote. Lugha ya matusi inayotumiwa na Polisi inaashiria pia ule uduni wa mwanamke mbele ya umma wa kiume. Anapaswa kuzungumziwa vile kwa sababu yeye ni mwanamke. Kule kumuuliza Mwavita ikiwa mimba aliyokuwa nayo ni ya mumewe, ni ishara ya mielekeo hasi waliyo nayo wanaume wengi kwamba wanawake si viumbe wa kuaminika.

Wakili wa Kinaya naye amesheheni taasubi za kiume. Kwa mfano, analikubali wazo la kumpiga mke kama wajibu wa mume kwa mke mtesi.

Anasema, "Hiyo ndiyo dawa pekee ya tangu zama za mababu zetu, wamefanya hivyo miaka nenda miaka rudi" (uk. 77). Ingawa jamii nyingi za Kiafrika huchukulia kitendo cha kumpiga mke kama dalili ya mapenzi na njia ya kumrudi mke, tabia hii imepigiwa maswali na makundi mbalimbali ya watu, hususan wale wanaozingatia masuala ya kike na haki za binadamu.

Hakimu anavumilia jambo hili pia kutokana na jinsi yeye binafsi alivyolelewa. Haoni kwamba ni hatia inayostahili adhabu. Asasi hii ya sheria inampokonya Mwavita malezi ya mwanawe mchanga na kumkabidhi mumewe kwa kisingizio kuwa Kinaya ana nguvu za kiuchumi kumlea mwanawe. Hapa, mapenzi ya mama hayafikiriwi kamwe, mbali na uwezo wa kiuchumi alio nao pia Mwavita.

Katika muktadha huu basi, sheria za nchi zinatumiwa kumnyamazisha mwanamke na kumkumbusha kuwa yupo hapa duniani kumtumikia mwanamume; kumzalia watoto na kumtimizia faraja zake.

### 2.5 *Uhuru wa Mwanamke*

Nadharia ya uchanganuzi - nafsia inaweza kutumiwa kama changamoto katika kuibua hisia za wanawake dhidi ya maonevu wanayokumbana nayo katika jamii.

*Mama Ee* ni kielelezo kizuri cha jinsi asasi za kijamii zinavyotumiwa kumnyima mwanamke uhuru wa kibinafsi. Ijapokuwa mwanamke huheshimiwa pale anapoolewa, heshima hiyo haina maana iwapo anaishi maisha ya utumwa. Tofauti yake na mtumwa halisi ni kwamba mtumwa anajua kuwa yeye ni mtumwa lakini mke aghalabu hajui kuwa yeye ni kama mtumwa.

Kupitia kwa wahusika wake, Mwachofi amezichunguza ada za kijamii na kubainisha jinsi zinavyomnyima mwanamke nafasi ya kuishi kama binadamu huru aliyekamilika. Kupitia kwa Wahusika Mwavita na Tenge, mwandishi ametuonyesha mwanamke anaweza kujisimamia mwenyewe kimaisha. Aidha, anaweza kufikia upeo wa maisha yake bila kumtegemea mwanamume.

Kupitia kwa mhusika Mwavita, tabia za "kike" ambazo mwanamke anapaswa kuwa nazo zinapigiwa maswali (uk. 58). Mwavita anaona kuwa tabia hizo zitapunguza utu wake na hisi zake kama binadamu. Hapa, anataka kuishi kama binadamu huru, wala sio kujifanya "mwema" na huku

anaidhiki nafsi yake. Hizi ni zile tabia zisizo na uhalisi wowote anazotakiwa kuwa nazo ili aweze kvyema katika mfumo ulioghoshi nguvu na mamlaka ya kiume. Mwavita anauliza, "kwani kutaka kuwa mtu na kuheshimiwa kama mtu ndio kujitia uume"! (uk. 59).

Mwandishi anaunda chama cha kina mama ambacho kinaweza kutumiwa kulishawishi bunge kubadilisha sheria zinazomdhalilisha mwanamke. Hata hivyo, mwandishi haoni kuwa wanawake watafika mbali ndani ya umoja huo. Hii ni kwa sababu chama hicho kinaongozwa na mabibi wa mabwanyenye ambao tayari wamekubali utumwa wa kimwili na kiroho.

Mabibi hao wamekolea wosia wa mwanakupona kiasi cha kwamba wanapohadithiwa taabu za akina mwavita na Tenge, hawaelewi na wala hawataki kuelewa (uk. 94).

Mwandishi ameonyesha pia kwamba haitoshi mwanamke kufikiriwa kama pambo na tumishi wa mwanamume pekee (uk. 96). Anatoa shime ya umoja wa wanawake utakaowawezesha kutambua haki zao. Hawapaswi kutiwa uwete na unyonge na wanaume, au kuitikia mambo tu bila kusaili. Udadisi wa mambo ni kimelea kitakachowawezesha kutambua haki zao kama binadamu.

2.6 *Mtazamo wa Mwandishi*

Mwandishi Mwachofi anaonekana kuegemea katika harakati za ukombozi wa wanawake zenye siasa kali (radical feminism). Nimemweka katika tapo hili kwa sababu kadha. Kwanza mtazamo wa waitifaki wa tapo hili unaelekea kutoa rai kwamba familia ni asasi ya kijamii iliyoteuliwa kuendeleza ugawaji wa rasilmali usio sawa baina ya wanawake na wanaume. Kwa ufupi, familia ni asasi inayoendeleza utabaka na udunishaji wa mwanamke.

Pili, wanashikilia kwamba tangu azali, wanaume ndio chanzo cha dhuluma zote dhidi ya wanawake, kwa hivyo ndio maadui wa wanawake. Tatu, wanashikilia kwamba umbo la mwanamke hususani uwezo wa kupata mimba na kuzaa ni jukumu la kishenzi ambalo linaweza kutupiliwa mbali. Badala yake, njia za uzalishaji mnemba zinaweza kuimarishwa ili wanawake waondokewe na jukumu hili linalowadhalilisha na kuwafanya wadunishwe na wanaume.

**3. Hitimisho**

Katika makala hii, nimeshughulikia kwa ufupi nadharia ya Uchangamuzi - nafsia katika muktadha wa masuala ya kike na kuonyesha jinsi inavyoweza kutumiwa kuhakiki kazi za kifasihi.

Tamthilia ya *Mama Ee* ni kielelezo kizuri cha mwandishi wa kike anayeandika kama mwanakundi maalumu la kijamii linalodhulumiwa. Kwa hivyo anaandika kazi ambayo imeathiriwa na ile hali ya kuwa yeye ni mwanamke, na kama mwanamke, ana nafasi aliyotengewa na jamii yake. Kwa kiasi kikubwa, mwandishi amefaulu kuibua zile nguvu za kile zilizofichika. Amejaribu kuonyesha kuwa kugubikwa kwa nguvu hizi na mifumo ya ugandamizaji wa mwanamke humnyima uhuru wa kuzifichua na kuzidhihirisha. Nguvu hizo za kike (female libido) basi ndizo zinazomhakikishia kiumbe huyu uhuru wa kibinadamu, sawa na mwanamume.

Kwa vyovyote vile, nadharia ya uchanganuzi - nafsia huweza kutumiwa kama kurunzi ya kumulikia mawazo ya mwanamke, na jinsi yanavyokuzwa na kuendelezwa katika jamii za kuumeni.

Wahusika waliotumiwa basi, ni vielelezo vya mawazo, falsafa na imani ya mwandishi kulingana na tajiriba yake mwenyewe katika jamii. Ni bayana kwamba taathira za mazingira ya mwandishi zimebainika kupitia kwa zao hili la kifasihi na kwamba taathira hizi zina uhusiano wa moja kwa moja na mfumo wa jamii.

Kwa kuhitimisha, ningependa kutoa rai kwamba ipo haja ya waandishi wa sasa na baadaye katika fasihi ya Kiswahili, kuwa na mtazamo mpya katika kusawiri wanawake. Ipo haja ya kuzikomoa itikadi za kuumeni kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii hasa pale wanapoandika kazi zao. Hawana budi kumwangalia mwanamke kama binadamu katika ujumla wake. Mwanamke asionekane kwamba anaongozwa na mwanamume katika kila hatua anayopiga maishani. Aangaliwe kama mwenzi wa mwanamume mwenye haki sawa na mwanamume.

**Marejeo**

Ba, M. (1980): *So Long a Letter,* Heinemann Biblia Takatifu, United Bible societies (1989).Revised.

Bouchier, D. (1983): *The Feminist Challenge,* London, Macmillan Press Ltd.

Eagleton, M. (1986): *Feminist Literary Theory*: A Reader, new York, Basil and Blackwell.

Figes, E. (1978): *Patriarchal Attitudes,* London, Virago Limited.

Maclaughlin, A. na Braxton (Wahariri) (1990): *Wild Women in the Whirlwing: Afro-American Culture and Contemporary Literary Renaissance,* New Brunswick, Rutgers Univesity Press,

Mule, K. (1991): "Swala la Mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili. Waandishi wa kike katika njia panda". Tasnifu ya M.A., chuo Kikuu, Kenyatta, Nairobi (Haijachapishwa).

Mwachofi, K.a. (1987): *Mama Ee,* Nairobi, Heinemann.

Nabhany na Amina (1972): *Sanaa ya Utungo: Utendi wa Mwanakupona. Utendi wa Ngamia na paa, Nairobi, Heinemann.*

Weedon, C. (1991): *Feminist Practice and Post Structuralist Theory,* Oxford, Basil Blackwell Ltd.